VIDEO YA MUONGOZO WA MAFUNZO:
Karibuni Nchini Mwetu

MUHTASARI

Video ya Ukaribisho katika Canada inajaribu kutoa utambulisho wa utajiri mkubwa wa maadili ya wenyeji na maoni yao huku ikionyesha baadhi ya matukio ya kihistoria yenye utata ambayo yameunda sura ya nchi hii na mahusiano kati ya wenyeji na wasio wenyeji.

Baada ya kuangalia video, tuna matumaini utakuwa na ushawishi wa kuendelea kujifunza zaidi kuhusu wenyeji wa Canada. Video hii ya muongozo wa mafunzo inayoambatanishwa inatoa maelezo zaidi, inapendekeza viunganisho na misamiati kukusaidia kuongeza ufahamu wa wenyeji wa Canada. Tunatunaini utatumia muongozo huu kama chanzo cha kupata mafunzo zaidi.

Canada inaainishaje wenyeji? Kipengele cha 35 (2) cha Katiba ya Canada ya mwaka 1982 inaainisha watu wa kale kujumuisha "Wahindi", "Wainuit" na "Wamétis" wanaopatikana Canada.

Jina "Wahindi" linachukuliwa kama neno la kikoloni lenye kukera. Neno **wenyeji** pia linapendelewa kuliko watu wa kale wakati wa kujadili wa wenyeji wa Canada.

Mataifa ya Mwanzo ni jina linalohusisha wenyeji ambao hawatambuliki kama wainuit au wamétis.

- *en.wikipedia.org/wiki/Indigenous_peoples_in_Canada*

Wainuit ni kundi la wenyeji wanaoishi katika jumuiya 53 ndani ya maeneo ya aktiki ya Canada, Grinilandi na Alaska. Kihistoria Wainuit walijulikana kama "Waeskimo", lakini jina hili ni la dharau, na halipaswi kutumika.

- *en.wikipedia.org/w/Inuit*

Métis inatokana na neno la kifaransa lenye maana ya "kuchanganya". Ni kundi maalum la wenyeji ambalo kizazi chake ni mkusanyiko wa Mataifa ya Mwanzo na watu wa ulaya. Wazao wao walijulikana kama "machotara" ambalo halitumiki tena na linachukuliwa kama la uchokozi.

- *en.wikipedia.org/wiki/M%C3%A9tis_in_Canada*

KATIKA VIDEO

Hadi 2016, Canada ilikuwa na wenyeji 1,673,785 ambao nia asilimia 4.9% ya idadi ya wakazi wote. Leo hii Canada kuna kadri ya Mataifa ya Mwanzo tofauti tofauti yapatayo 634, na karibia makundi ya lugha 60 tofauti wanaoishi Canada katika majimbo ya asili na mijini.

- *en.wikipedia.org/wiki/First_Nations*

Katika video umetambulishwa na kukaribishwa na wawakilishi sita wa wenyeji kutoka pote Canada. Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu hawa wenyeji kupitia viunganisho vifuatavyo:

GWAYEE (BRITISH COLUMBIA – MATAIFA YA MWANZO)

- *kingcome.ca*
- *youtube.com/watch?v=0CIB00xJkiY*

INUVIK (MAJIMBO YA KASIKAZINI MASHARIKI – WAINUIT)

- *inuvik.ca/en/index.asp*
- *en.wikipedia.org/wiki/Indigenous_peoples_in_Northern_Canada*

PENTICTON (BRITISH COLUMBIA – MATAIFA YA MWANZO)

- *syilx.org/about-us/syilx-nation*
- *pib.ca*

MATAIFA SITA (ONTARIO)

- *sndevcorp.ca/history-of-six-nations*
- *en.wikipedia.org/wiki/Six_Nations_of_the_Grand_River*

UNAMA'KI (RASI YA BRETON, NOVA SCOTIA)

- *cbu.ca/indigenous-affairs/mikmaq-resource-centre/mikmaq-resource-guide/historical-overview*

ÎLE-A-LA CROSSE, (SASKATCHEWAN – WAMÉTIS)

- *en.wikipedia.org/wiki/%C3%8Ele-%C3%A0-la-Crosse*

Kama umeangalia video hii ukiwa Canada, fikia na jifunze zaidi kuhusu Mataifa ya Mwanzo katika jumuiya au mkoa wako. Unaweza kuanzia na google tafiti kuona mji wako upo kwenye jimbo lipi la watu wenyeji. Pia kurejea kwenye viunganisho vingine.

Wenyeji wana maadili na simulizi za kipekee. Historia na simulizi ni za muhimu katika kuhifadhi utamaduni na utambulisho wa wenyeji. Mara nyingi watu mahsusi katika jamii wanachukua majukumu ya kuhifadhi historia za simulizi kwa umakini mkubwa. Wenyeji hufundishana maadili na historia kati ya vizazi kwa njia ya kusimuliana. Wenyeji pia hueleza hadithi na historia kwa njia ya vitu vya ishara na lugha ya ishara kama vile milingoti ya sanamu na milingoti ya nyumba.

Kila tamaduni, jamii, na hata familia ya wenyeji ina mila na hadithi za kale, nyimbo au ngoma za kipekee. Tamaduni tofauti zina sheria tofauti za miliki. Baadhi ya nyimbo, majina, ishara, alama au ngoma zinamilikiwa na baadhi ya watu au familia na haziwezi kutumika, kusimuliwa upya, kuchezwa au kuimbwa bila idhini.

MATUKIO MUHIMU

Mahusiano ya kihistoria kati ya wenyejii na wale ambao siyo wenyeji nchini Canada ni tatanishi na yameshawishiwa na ukoloni, matukio ya kihistoria, sheria na mtazamo wa ubaguzi. Matukio haya yameunda maswala ya siku hizi yanayohisiwa na wenyeji. Lakini kuna mikakati inayofanyika Canada ili kuboresha na kushughulikia mabaya ya huko nyuma.

Sehemu hii ya mwisho ya muongozo wa mafunzo inajaribu kutoa maelezo zaidi kuhusu matukio muhimu ya kihistoria yaliyogusiwa kwenye video.

UKOLONI

- *en.wikipedia.org/wiki/History_of_Canada*

Kabla watu wa ulaya hawajafika, Amerika ya Kaskazini ilikuwa inakaliwa na wenyeji wakiishi kwa ufanisi katika mila zao maalamu, lugha, na jinsi ya kuelewa. Wenyejii wameishi sasa inayoitwa Canada kwa zaidi ya miaka 10,000.

Waingereza na Wafaransa (wanaodaiwa kuwa waasisi wawili wa taifa la Canada) walikuwa wanapigana kudhibiti Amerika ya Kasikazini ambayo waliiona kama tajiri ya mali ghafi. Watu wa Ulaya walipowasili Amerika ya Kasikazini, waliichkulia kama ni nchi isiyokuwa na mwenyewe. Watu wa ulaya walishinikiza maadili ya tamaduni zao, dini, sheria, na kutunga sera zilizowapendelea; baadhi hawakuamini kuwa wenyeji ni watu.

Matokeo yake, kanuni na imani za watu wa ulaya zimepenyeza kwenye taasisi na sera za Canada kwa mtindo wa taratibu na ubaguzi wa kitaasisi. Kazi kubwa leo ni kuhusu kurekebisha mabaya ya nyuma na kusitisha madhara ya ubaguzi na uonevu.

KANUNI YA KIHINDI, 1876

- *en.wikipedia.org/wiki/Indian_Act*

Kanuni ya Kihindi ni sheria ya shirikisho inayobaini jinsi hifadhi na makundi ya wenyeji zinaweza kufanyakazi na ina ainisha nani anatambulika kama "Muhindi". Kanuni ya Kihindi ilikuwa ni njia nyingine ya kuwaingiza watu wa Mataifa ya Mwanzo kwenye jamii ya Ulaya haraka iwezekanavyo. Kanuni inajumuisha vipengele tofauti kama vile jinsi Wahindi walipata na kupoteza hadhi yao, hadhi ya kisheria ya wanawake, ukombozi, n.k. Kanuni ya Kihindi bado inatumika mpaka leo na bado ni kikwazo cha sheria kwa wenyeji.

Hifadhi: Kuwasili kwa watu wa Ulaya na wao kufanya makazi, watu wa Mataifa ya Mwanzo na watu wa Ulaya waliingia kwenye mfarakano kuhusu nani atatawala ardhi na rasilimali hizi. Watu wa Mataifa ya Mwanzo waliwekwa kwenye maeneo madogo ya ardhi yaliyoitwa hifadhi. Wengi wa Mataifa ya Mwanzo wanaendelea kuishi kwenye hifadhi ndogo, ambazo zinamilikiwa na serikali. Hili limekuwa chanzo cha migongano kati ya wenyeji na serikali.

SHULE ZA MAKAZI

- *en.wikipedia.org/wiki/Canadian_Indian_residential_school_system*

Moja ya urithi wa Kanuni ya Kihindi unaosumbua ni ulazima wa kuhudhuria kwenye shule za makazi. Kulikuwa na shule za makazi ya Kihindi 140, zilifadhiliwa na serikali na kuendeshwa na makanisa. Zaidi ya watoto 150,000 wa wenyejii walilazimishwa kuhudhuria shule hizi. Serikali ilitaka kuwaunganisha wenyeji kwenye jamii ya Canada-Ulaya.

Watoto wa wenyeji walichukuliwa kutoka kwa wazazi na familia zao na kulazimishwa kuachana na lugha, imani zao na desturi za kitamaduni. Tarehe 11 Juni 2008, Serikali ya Canada ilitoa radhi rasmi kwa wahanga wa shule za makazi. Unaweza kuona nakala ya radhi iliyotolewa na Waziri Mkuu kupitia kiunganisho kifuatacho:

- *rcaanc-cirnac.gc.ca/eng/1100100015644/1571589171655*

WANAWAKE NA WASICHANA WENYEJI WALIOUAWA NA KUPOTEA

- *mmiwg-ffada.ca/final-report*

Septemba 2016, Serikali ya Canada ilianzisha uchunguzi wa kitaifa wa upoteaji na mauaji ya wanawake na wasichana wenyejii (MMIWG). MMIWG inaashiria mgogoro wa haki za binadamu kutokana na upoteaji na mauaji ya wanawake wenyeji kati ya mwaka 1980 na 2012. Makundi ya wanawake ya wenyeji iliweka takwimu kwenye nyaraka za waliopotea na kuuawa kuwa 4,000. Kuongezeka kwa uamsho kumepelekea uungwaji mkono kwa familia na jamii za wenyejii na kuunganisha watu kwa lengo moja la kudai haki.

KUJENGA WAKATI UJAO ULIOBORA

TUME YA UKWELI NA MARIDHIANO (TRC)

- *cbc.ca/news/politics/truth-and-reconciliation-94-calls-toaction-1.3362258*

Serikali ya shiriksho iliunda Tume ya Ukweli na Maridhiano (TRC) mwaka 2008 kuchunguza urithi wa shule za makazi. Kazi ya TRC ilikuwa ni kukusanya, kuchapisha na kuweka kumbukumbu za wahanga 80,000 wa shule za makazi ili wahanga waweza kuanza uponywaji wa viwewe vya matukio haya.

Mwaka 2015, Tume ya Ukweli na Maridhiano ilitoa ripoti yake ya mwisho na kuchapisha miito ya kuchukua hatua 94, ikihimiza ngazi zote za serikali kufanyakazi pamoja kubadili sera na programu katika jitihada za pamoja za kurekebisha madhara yaliyosababishwa na shule za makzi na kusonga mbele na maridhiano.

Kazi ya TRC haikuwa tu kuweka kumbukumbu hasa za sehumu ngumu ya historia ya Canada ila ilijikita katika imani ya kusema ukweli kuhusu historia ya wenyeji na wasio wenyeji kutupatia mwanzo bora katika kujenga wakati ujao uliobora. Ni mwanzo wa aina ya matumaini mapya.

Nyingi ya dhana mbaya na matatizo hutokea wakati watu hawaelewi ukweli, au habari zozote kuhusu watu wenyeji. Tunakuhimiza kutafuta maelezo: Soma “Miito ya Kuchukua Hatua” ya TRC, tembelea kituo cha Urafiki; soma vitabu vilivyotungwa na wenyeji; chunguza Sanaa zilizotengenezwa na mafundi wa wenyeji; chukua darasa kuhusu watu wenyeji; Tengeneza kikundi kazini kwako kuzungumzia maswala ya wenyeji; shiriki katika matukio kama Matembezi ya Maridhiano na Siku ya Taifa ya Wenyeji nchini kote Canada.

Tunahitaji kufanyakazi pamoja na kuungana mkono katika kutengeneza sehemu ambapo watu wote wanaheshimika na kushirikishwa. Maridhiano ni safari ya mtu binafsi ambamo kila Mcanada lazima ashiriki.

Huu muongozo umetengenezwa na Kory Wilson kwa niaba ya ISSofBC kama kiambatisho cha video ya Karibu Canada. Muongozo umepewa leseni CC BY NC 4.0 labda ionyeshe vinginevyo. Leseni hii inakupa fursa ya kuchanganya, kurekebisha na kutumia kama msingi kutengeneza kazi ambayo siyo ya biashara. Kazi yako mpya lazima kutambua Kory Wilson na iwe siyo ya biashara. Tafadhali tumia taarifa kwa maelezo: Karibu kwa Muongozo wa Mafunzo wa Canada uliotungwa na Kory Wilson, unapatikana chini ya Maelezo Ubunifu kwa Wote-Leseni isiyo ya kibiashara ©2019, Kory Wilson.